Kushirikisha Wasiwasi Wako

Wasimamizi wa shule wanataka kuweka wanafunzi na wafanyakazi salama na wanataka kusikia wasiwasi wako na kufuatilia kama inavyotakiwa.

Wakati wowote kama una wasiwasi kuhusu mwingiliano baina ya wafanyakazi au wanaojitolea na wanafunzi una haki ya kuongea kuhusu tukio na wasimamizi wa shule. Hata kama utasita au kwa sababu nyingine hautaki kutangaza uongo au hautaki kumharibia mtu sifa zake nk. Ni vizuri kuongea na kuweka sawa usalama na kutoa wasiwasi.

Unakaribishwa na unahamasishwa kuleta wasiwako kwa mkuu shule, msaidizi wa mkuu wa shule, mkurugenzi wa michezo au kwa idara ya uajiri katika shule/wilaya kwa kupiga simu 503-399-3061. Unaweza kuwasiliana nao kupitia simu, email (barua pepe) au barua. Na kama utapenda kutoa taarifa, unaweza kufanya hivyo kwa kubaki sirini, tafadhali jisikie kufanya hata hivyo. Ingawa, tungependa kukuomba kuwa unaacha taarifa maalum (nani alihusikia, lini, wapi n.k) kadri uwezavyo ili tuweze kufanya uchunguzi na kuchukua hatua zinazotakiwa.

Unashauriwa kuwa unaangalia mawasiliano ya kwenye mtandao kwa mwanafunzi wako na utoe taarifa mara moja kwa uongozi wa shule kama utakuta kitu chochote au una wasiwasi. Rasimali kuhusu kuwaweka wanafunzi salama kwenye mtandao unaweza kupata hapa www.salkeiz.k12.or.us/parents/child-abuse-prevention.

Na kama utahisi kuwa mtoto ananyanyaswa, unahamasishwa mara moja kuwasiliana na idara ya huduma za jamii na unanyanyasaji wa watoto Oregon kwa kupiga simu 1-855-503-SAFE(7233) au wakala wa vyombo vya sheria

Shule za umma za Salem-Keizer zinathamini ushirikiano wako katika kumlinda mwanafunzi. Kwa pamoja, tunaweza kuweka mazingira salama kwa wanafunzi na watu wazima.

LEARNING FOR A LIFETIME
SALEM•KEIZER PUBLIC SCHOOLS

Salem-Keizer Public Schools is an affirmative action/equal opportunity institution.

SALEM-KEIZER PUBLIC SCHOOLS

Mwingiliano na mwongozo kwa WAFANYAKAZI na WANAFUNZI



HUM-W039 Rev. 1.20

JUKUMU Letu Sisi KWAKO

Shule za umma za SALEM-KEIZER linajukumu la kutoa mazingira yenye afya na salama kwa wanafunzi wanaposhiriki katika shughuli za wilaya. Na kujifunza kama kunatokea wakati wa shule au wakati wa shughuli za ziada, usalama ni kipaumbele kwetu.

Shule za umma za Salem-Keizer zimeanzisha matarajio kwa wafanyakazi, wakandarasi, wakala na wanajiotelea katika kukuza usalama kwa wote watu wazima na wanafunzi. Wanafanyakazi wanakubaliana na huu mwongozo na inaonyesha ni muhimu kuwashirikisha wazazi.

Kuhusiana mawasiliano ya kwenye mtandao wafanyakazi wanategemewa:

- Kuweka akaunti tofauti kati ya binafsi na taaluma kwenye mitandao ya jamii
- Kukataa urafiki au kufuatilia ombi kutoka kwa mwanafunzi kwenye akaunti binafsi ya mitandao ya kijamii, na siyo kutuma ombi la urafiki au kufuatilia ombi kwa mwanafunzi kutoka akaunti binafsi. Hii haimaanishi kuwa mfanyakazi hampendi mwanafunzi bali ni kuweka mipaka.
- KUTO kuwasiliana kupitia maandishi, mitandao ya kijamii au vifaa vingine vya teknolojia ambavyo wanafunzi wanatumia jukwaa la simu binafsi. Wanafanyakazi wanaweza kuwasiliana na wanafunzi na wazazi kupitia njia inayoitwa "Synergy ParentVUE" "Syngery StudentVUE" na kuwakumbusha jukwaa mahasusi kwa wilaya kwenye maandishi. Mawasiliano yote na mwanafunzi yanatakiwa yawe wazi na kuhusu shule au usalama tu.

Kuhusiana kuendesha wanafunzi mfanyakazi HAWEZI:

- Kumuendesha mwanafunzi au wanafunzi kwa usafiri binafsi bila kuruhusiwa na utawala wa shule. Mfanyakazi wakati mwingine anaweza kuendesha basi kupakia kikundi cha wanafunzi kwenda kwenye shughuli za shule. Ni lazima kuwepo watu wazima wawili au wanafunzi wawili katika gari wakati wote.
- Kutoa mafunzo ya kuendesha gari, pale tu itakapo ruhusiwa kwenye programu ya elimu.

Kuhusiana mahusiano na wanafunzi, wafanyakazi wanatakiwa:

- Kutenga wazi maisha yao binafsi na taaluma na kuweka mipaka baina ya wanafunzi na familia.
  Kwa mfano, Inakuwa si jambo zuri kwa mfanyakazi kwenda matembezi au likizo pamoja na familia ya mwanafunzi. Ingawa hizi aina za mawasiliano zinaweza zisionekane siyo nzuri pale ambapo mahusiano ya muda mrefu yateendelea kati ya mfanyakazi/mtu wa kujitolea na familia ya mwanafunzi au mahusiano yakatokea nje ya mazingira ya shule.

  Mahusiano mapya yanaweza kutokea kupitia mfanyakazi, mwanafunzi na familia kupitia shughuli zinazohusu shule, ingawa wanafunzi watu wazima wanatakiwa kuwa na nidhamu na wazi.
- SIYO kuzuia urafiki pamoja na wanafunzi au familia ambao umeanzia nje na mazingira ya shule (kama, makanisani, majirani, vikundi n.k) kupita matarajio ya wilaya(shule) Kwamfano kocha au mwalimu kumuondoa mtoto wako kwenye ukurasa wa Facebook, hata kama ni rafiki wako wa karibu. Hii nikuhakikisha kuwa hakuna upendeleo unaodokeza kwa mwanafunzi.

Kuhusiana zawadi na upendeleo maalumu, mfanyakazi anatakiwa:

- Tengeneza mazingira ya uwazi na mfumo wa haki ambapo wanafunzi wote wanapata nafasi sawa katika kupata cheti, kadi ya zawadi, jalada au utambuzi mwingine. Wafanyakazi wasipokee au kutoa zawadi au upendeleo maalumu.

Kuhusiana na timu au kusheherekea darasani mfanyakazi HATAKIWI:

- Kufanya sherehe nyumbani kwao. Matukio ya vikundi yanatakiwa kupata kibali na kuruhusiwa na msimamizi wa shule na kusimamiwa na watu wengi wazima

Kuhusiana na kuongea na mwanafunzi moja moja mfanyakazi HATAKIWI:

- Kukutana na mwanafunzi pekee yake kwenye eneo la siri. Mfanyakazi anatakiwa kuwa makini na mazingira na kukwepa maongezi na wanafunzi ambayo yanaweza kutafsiriwa vibaya.

Kuhusiana faida na fedha mfanyakazi HATAKIWI:

- Mfanyakazi hatakiwa kujinufaisha kifedha kutokana na mahusiano ya wanafunzi na wazazi.